

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

Anwani ya simu: "MAKAMU",  
Simu Na.: +(255)026 2329006  
Nukushi.: +(255)026 2329007/2983150  
Barua Pepe: km@vpo.go.tz



Mji wa Serikali,  
Eneo la Mtumba,  
S. L. P. 2502,  
**40406 DODOMA,**  
TANZANIA.

**20 Septemba 2025**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Philip Mpango, leo tarehe 20 Septemba 2025 ameondoka nchini kuelekea New York, nchini Marekani kumwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika Kikao cha 80 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA 80).

Kikao cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kinachoshirikisha Wakuu wa Nchi na Viongozi mbalimbali ni Mkutano muhimu ambao, pamoja na mambo mengine, hujadili masuala ya kiuchumi, kisiasa na haki za binadamu.

Kikao hicho kinafanyika chini ya Kaulimbiu isemayo **"Tuko Vizuri tukiwa pamoja: Miaka 80 na Zaidi kwa Amani, Maendeleo, na Haki za Binadamu"** (*Better Together: 80 Years and Beyond for Peace, Development, and Human Right*). Kaulimbiu hiyo ni wito wa pamoja wa kuimarisha Umoja wa Mataifa ili uweze kukabiliana vyema na changamoto za sasa na zile zinazokuja, huku ukilinda mafanikio yaliyopatikana.

Aidha, Mheshimiwa Makamu wa Rais anatarajiwa kuhutubia Kikao cha 80 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa pamoja na kushiriki kwenye vikao mbalimbali ikiwemo Mjadala Mkuu (*General Debate*), Mikutano ya pembezoni na Mikutano ya uwili.

\_\_\_\_\_  
Franco Singaile  
Msaidizi wa Makamu wa Rais - Habari